



TANGAZO LA UFADHILI KWA MWAKA WA MASOMO 2016/2017 MAFUNZO YA ASTASHAHADA YA UUGUZI NA UKUNGA (CERTIFICATE IN NURSING AND MIDWIFERY)

1. Usuli

Shirika la Amref Health Africa Tanzania, linawakaribisha waombaji wanaopenda kusomea astashahada ya uuguzi na ukunga (Certificate in Nursing and midwifery) inayotolewa na vyuo mbalimbali nchini Tanzania. Programu hii imeanza rasmi mwaka 2012 na tayari wanafunzi takribani 54 wamehitimu mafunzo na sasa wahitimu 10 wameajiriwa na wanatoa huduma katika wilaya ya Kilindi na Mtwara and zaidi ya wanafuzi 251 wamefaidika na ufadhili huu.

Lengo la kutoa ufadhili ni kuongeza idadi ya wauguzi wakunga katika maeneo ambayo watoa huduma hii ni wachache na vifo vya mama na mtoto vipo kwa kiwango kikubwa.

2. Mkoa unaopewa Kipaumbele kuomba ufadhili.

Nafasi hizi ni kwa wale wanafunzi waliomaliza kidato cha NNE na wenye sifa za kujiunga na cheti cha uuguzi kutoka mkoa wa Geita.

3. Masharti ya kujiunga na kozi

Masharti ni kama yafuatayo.

- i. Uwe umedahiliwa na NACTE kwenye chuo chochote cha uuguzi Tanzania
- ii. Uwe tayari kuingia mkataba wa kufanya kazi katika halmashauri utakayopangiwa katika mkoa tajwa na kutii masharti ya mkataba kwa muda usiopungua miaka mitano.
- iii. Uwe unatoka katika familia ya kawaida. Tutahitaji uthibitisho kutoka kwa mwenyekiti wa kijiji au mtaa kuhusu uwezo wa uchumi wa familia. Nafasi hizi

zinalenga zaidi kusaidia watoto wanaotoka katika familia duni kiuchumi.

- iv. Ufadhili huu hautolewi kwa mtoto ambaye mzazi wake au mlezi ni mtumishi wa serikali au sekta binafsi au mfanyabiashara mkubwa.

4. Aina ya ufadhili

Wote watakao chaguliwa watalipiwa gharama zote zitakazohitajika na chuo kwa muda wa miaka miwili. Wazazi na walezi watachangia gharama za kujikimu watoto wao pamoja na nauli zao kwa kipindi chote.

5. Namna ya kutuma maombi

Maombi yatumwe kwa **mkono** kwenye Ofisi za Amref za Geita zilizoko Karibu na ofisi za halmashauri ya wilaya ya Geita. Mwombaji atumie anuani hii: Meneja Miradi- Kujenga Uwezo, Amref Health Africa-Tanzania, na iandikwe juu ya bahasha **Maombi ya Ufadhili 2016/2017.**

Barua za maombi zipitishwe na Wenyeviti wa Vijiji husika. Unatakiwa kuonesha kama umekwisha omba kujiunga na chuo au umeshapata nafasi ya kujiunga na chuo kwa 2016/2017

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30 Agosti **2016. Uhakiki wa waombaji utafanywa na uongozi wa wilaya husika. Hivyo waombaji wote waweke namba zao za simu kwa ajili ya kuitwa kwa usaili.**

6. Terehe ya kuanza na muda wa kozi

Tarehe ya kuanza masomo itatolewa na wizara na muda wa masomo ni miaka miwili.

Kwa maulizo, tafadhali wasiliana na:

Amref Health Africa, Tanzania

Barabara ya Ali Hassan Mwinyi; S.L.P 2773, Dar es Salaam,

Namba za Simu: +255 22 2116610/2131981/2136731/2153104; Namba ya Faksi: +255 2115823;

au +255 716 533115/0757451032

Barua Pepe: courses.tanzania@amref.org; Tovuti: www.amref.org